SHULE YA SEKONDARI DEOSANGA

S.L.P 178

MAKAMBAKO

TAR……...

Kumb.Na. DSS/F.1 /REG./ 2021/02

JINA LA MWANAFUNZI…….....

S.L.P……

MAKAMBAKO.

YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DEOSANGA,HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO,WILAYA YA NJOMBE-MKOA WA NJOMBE.

1.0. **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari **DEOSANGA.**Shule ipo umbali wa kilomita moja (**KM 1)** kutoka ofisi ya Halmashauri ya Mji Makambako upande wa magharibi.Shule ipo karibu na uwanja wa soko la kimataifa (Karibu na shule **ya Msingi Mashujaa**).Shule hii ni ya **kutwa** pia mchanganyiko (wavulana na wasichana).

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** .Wanafunzi wote mnatakiwa kuripoti tarehe **11/01/2021 na si vinginevyo.** Aidha hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayemchelewesha mwanafunzi kuripoti shule.

Mwanafunzi anatakiwa kufika siku hiyo akiwa na mzazi/ mlezi wake pamoja na fomu zilizoambatanishwa zikiwa zimejazwa vizuri.

1.2 Pamoja na barua hii pia nimeambatanisha fomu zifuatazo;

A) FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI.

B) SHERIA ZA SHULE.

C) FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.

D) FOMU YA AFYA YA MWANAFUNZI(IJAZWE NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALI TU)

E) MSHONO WA SARE YA SHULE KWA AJILI YA WASICHANA (UMEAMBATANISHWA)

NB.FOMU A,C, D ZIJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI.

Kwa niaba ya Bodi ya Shule na wanajumuia wote wa **Shule ya Sekondari DEOSANGA** ni mategemeo na matumaini yangu kwamba utanufaika na elimu itakayo kupelekea kupata maendeleo yako, jamii yako na taifa kwa ujumla.

Shule ina matarajio kwamba utakuwa na juhudi katika masomo,tabia njema, ari ya kujifunza, ushirikiano na walimu,watumishi wasio walimu na wanafunzi wenzako kwa ujumla.

Hongera na karibu sana katika Shule ya Sekondari Deo Sanga.

……

ZUBERI J.KILINGO
MKUU WA SHULE
0752648114.

2.0.**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

2.1. SARE ZA SHULE

1.WAVULANA

a) Suruali mbili (2) rangi ya dark brown pamoja na tai mbili (2) upana usipungue inchi 12 mshono wa marinda.

b) Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu

c) Viatu vya ngozi nyeusi visivyo na kisigino kirefu vya kufunga na kamba.

d) Soksi pea mbili (2) nyeusi ndefu.

e) Sweta rangi ya ugoro (dark brown).special, kama rangi ya kitambaa cha suruali.(**IWE NA LABEL ILIYOANDIKWA ISAKA)**

2.WASICHANA.

a) Suruali mbili (2) rangi ya DARK BROWN upana usipungue inchi 12.

b) Tai mbili (2) mshono wa marinda.

c) Vigauni viwili vyeupe (mshono umeambatanishwa) JINA LA KITAMBAA CHA KUSHONA GAUNI NI **HALWA**

d) Viatu vya ngozi nyeusi visivyo na kisigino kirefu vya kufunga na kamba.

e) Sweta rangi ya ugoro (darkbrown) special, kama rangi ya kitambaa cha suruali.**(IWE NA LABEL ILIYOANDIKWA ISAKA).**

3.VAZI LA WANAFUNZI WAISLAM (WASICHANA)

a) Kitambaa cha kichwani “hijabu”cheupe kisicho na urembo.

b) Suruali mbili rangi ya dark brown kitambaa kimeambatanishwa.

MIFANO YA MAVAZI YA WANAFUNZI

MWANAFUNZI WA KIUME

MWANAFUNZI WA KIKE

MWANAFUNZI WA KIKE BILA SWETA

MWANAFUNZI WA KIKE MUISLAM

4.**SARE ZA MICHEZO**

a) Tracksuit rangi ya bluu bahari wasichana na wavulana.

b) T-shirt rangi ya bluu wavulana na wasichana isiwe na maandishi ya aina yoyote.

c) Raba nyeupe na soksi zake.

5. **VIFAA VYA KITAALUMA (KUJIFUNZIA)**

a) Daftari kaunta books (quire 3) ziwe 9.

b) Daftari ndogo aina ya msomi ziwe 10 kwa ajili ya kufanyia mitihani ya kila wiki **(Weekly Test Examinations).**

c) Mkebe wenye vifaa vyote (Mathematical Tables).

d) Rula ya sentimita 30.

e) Kalamu za wino (bluu/ nyeusi na penseli za kutosha.

f) Jalada moja la plastic yanapatikana kwenye stationary kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake shuleni.

g) Mfuko (begi) la kubebea daftari.

6. USAFIRI

Mwanafunzi aandaliwe baiskeli ili imsaidie kuwahi shule kama anaishi zaidi ya **kilomita tatu** kufika shule.

7.**MICHANGO YA CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI WOTE.**

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutoa;-

b) Mahindi debe mbili (2)kwa mwaka au debe moja kwa nusu muhula.

c) Maharage aina ya SARUNDI Lita kumi kwa mwaka au lita tano kwa muhula.

d) Fedha taslimu kiasi kiasi cha **TSHS.30,000/=** kwa mwaka au **Tshs. 15,000/=** kwa muhula.Matumizi ya fedha hii ni kumlipa mpishi,ununuzi wa kuni,kukoboa na kusaga mashineni,kununua chumvi,kununua mafuta ya kupikia,mboga za majani, pamoja na mchele kama bajeti inaruhusu.**ZILIPWE KWENYE AKAUNTI**,**60310019316 NMB**. Jina la akaunti **EK.DEOSANGA SEKONDARI.**

8.**MAHITAJI MENGINE.**

1.Wavulana waje na;-

a) Rimu moja tu (01) ya karatasi kwa ajili ya kufanyia mitihani kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni.

b) Mfagio mmoja tu (chelewa) kwa ajili ya kufanyia usafi wa mazingira ya shule.

2.Wasichana waje na;-

a) Rimu moja tu (01) ya karatasi kwa ajili ya kufanyia mitihani kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni. b) Mfagio mmoja tu (chelewa) kwa ajili ya kufanyia usafi wa mazingira ya shule.

2.2 **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

2.3 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na.10** ya mwaka **1995**.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya **Rais-TAMISEMI** yenye jukumu la usimamaizi wa elimu na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kushiriki kwa makini katika kujisomea uwapo shuleni na wakati wa jioni ukiwa nyumbani kwenu.

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.

f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi, na mazingira ya shule.

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

i) Kutunza mali za umma.

2.4.**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA WEWE MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

a) Wizi

b) Uasherati na ushoga.

c) Ubakaji.

d) Ulevi,na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadharika.

e) Kupiga au kupigana

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau bendera ya taifa**.**

h) Kuwa mjamzito/kupata mimba **i**)Kuoa au kuolewa **j)**Kutoa mimba

k) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

m) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

A) TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1.Jina la mwanafunzi……..

2.Mahali alipozaliwa……..

3.Tarehe ya kuzaliwa……..

4.Dini……Dhehebu……

5.Shule ya msingi uliyotoka…….

6.Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile mpira wa miguu,mpira wa mikono,riadha, n.k …….....

7.Sahihi ya mwanafunzi…….tarehe……

B) TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI.

1. Baba yu hai…….ndiyo / hapana.

2. Mama yu hai……Ndiyo / hapana.

3.Jina la mzazi/ mlezi anayekulea…….

4.Uhusiano wako na mlezi…….

5.Kazi ya mzazi / mlezi……

6.Anuani ya mzazi / mlezi……Namba ya simu……

7. Mahali ambapo mzazi / mlezi anaishi;-

Mji…….kata……mtaa……Jina la barozi……..…Namba ya simu ……..……..Sahihi mzazi/ Mlezi……tarehe……

C) NDUGU WENGINE WA KARIBU WANOWEZA KUTAMBULIWA NA SHULE.

Na	JINA	UHUSIANO	ANUANI YAKO	SIMU

AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI.

A) MWANAFUNZI

Mimi ……(mwanafunzi) kidato cha …… nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote,sheria, na taratibu zote za shule nakubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari DEO SANGA.

Kwa hiyo naahidi kwamba;-

1. **Nitatii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.**
2. **Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo havitakiwi kunyume na uongozi wa shule na serikali kwa ujumla.**
3. **Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na mazingira,samani,(furniture),vitabu,Majengo ya shule,na kadharika.**

Sahihi ya mwanafunzi…….Tarehe……

B) MZAZI / MLEZI.

Mimi ……ninakubali mtoto wangu…….wa kidato cha ……..mwaka…….. Kujiunga na shule ya sekondari DEO SANGA kuanzia tarehe…….. akiwa wa kutwa.

Kwahiyo naahidi kwamba ;-

1.Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule,walimu,na wafanyakazi wengine katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu.Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingztia sheria,kanuni,na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.

Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema,kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulu kwa muda wote awapo shuleni.

Anuani yangu ya kudumu……..

Sahihi……..Tarehe……

FOMU YA AFYA YA MWANAFUNZI.

DEO SANGA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 178

MAKAMBAKO

DATE…./12/20...

THE MEDICAL OFFICER

…….

…….

REF:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please kindly examine (name)……to determine his / her physical and mental fitness for pursuing Secondary education studies.

……

ZUBERI J.KILINGO.

1.Eyesight……

2.Hearing…….

3.Spleen……

4.Limbs……..

5.Leprosy……..

6.Eplepsy……

7.Cardiac diseases……

8.Rheumatism……

9.Veneral diseases……..

10.Pregnancy……..

11.ANY OTHER SERIOUS DISEASES……..

General comments…….

Name……Signature……date……..Stamp……